**TAARIFA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. JENISTA JOAKIM MHAGAMA (MB.) KWA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU MAFANIKIO YA MWAKA MMOJA WA SERIKALI YA AWAMU YA SITA YALIYOPATIKANA KWENYE ENEO LA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, TAREHE 16/03/2022.**

***Ndugu wanahabari;*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetuwezesha kukutana hapa leo tukiwa na afya njema. Pia, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru kwa utayari wenu wa kushirikiana na Ofisi hii kila tunapowahitaji katika jukumu la kuwaelimisha na kuwafikishia wananchi taarifa muhimu zinazohusu masuala ya kiutumishi na utawala bora ili umma wa Watanzania uweze kuhabarishwa. Napenda kuchukua fursa hii tena kuwashukuru sana kwa mchango wenu huu mkubwa kwa ustawi wa Taifa.

***Ndugu Wanahabari;*** kama tunavyofahamu sasa hivi tuko katika kipindi cha kuadhimisha mwaka mmoja tangu Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu alipoingia

madarakani tarehe 19 Machi, 2021 baada ya kuondokewa na mpendwa wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli tarehe 17 Machi, 2021 aliyekuwa Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake Mahali Pema Peponi. Ameni.

***Ndugu Wanahabari;*** Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha mwaka mmoja imepata mafanikio makubwa katika eneo la Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mafanikio haya yanatokana na azma ya Mhe. Rais ya kutaka kuujenga utumishi wa umma wenye tija katika maendeleo ya taifa.

***Ndugu Wanahabari,*** naomba nichukue fursa hii kwa namna ya pekee kabisa kumpongeza kwa dhati Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa mafanikio makubwa ya utendaji wa kazi yanayoonekana katika sekta mbalimbali nchini. Mhe. Rais wetu amedhihirisha kuwa yeye ni kiongozi bora, muadilifu, mbobezi,

mzalendo, mchapakazi, mcha Mungu, mwenye nia na maono makubwa ya kuleta ustawi wa taifa na maendeleo ya Watanzania. Tunamuombea Baraka kwa Mwenyezi Mungu ampe afya njema na maisha marefu.

***Ndugu Wanahabari;*** Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ina jukumu la kisera la kusimamia uendelezaji sera katika Utumishi wa Umma, Utawala wa Utumishi wa Umma, Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Mishahara, Usimamizi wa Mifumo ya Uendeshaji wa Serikali, Usimamizi wa Mifumo ya Utendaji Kazi wa kila Siku Serikalini, Uendelezaji Rasilimaliwatu, Ukuzaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma, Usimamizi wa Serikali Mtandao na Usimamizi wa Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma. Ofis ya Rais pia ina dhamana ya kusimamia masuala ya Utawala Bora na Vilevile ina jukumu la kusimamia taasisi fungamanishi zinazoshiriki katika kuleta maendeleo na ustawi wa wananchi nchini.

***Ndugu Wanahabari;*** azma ya Mhe. Rais kuuboresha Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilijidhihirisha rasmi wakati akilihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 kwa mara ya kwanza tangu aapishwe kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo alisema kuwa Serikali anayoingoza itaendeleza jitihada za kuimarisha maadili, nidhamu uzalendo, uwajibikaji pamoja na kusimamia haki na stahiki za Watumishi wa Umma na Watendaji mbalimbali serikalini ili kuongeza moyo wa kufanya kazi kwa bidii na uwajibikaji wa hiari kwenye Utumishi wa Umma.

***Ndugu Wanahabari,*** kazi nzuri zilizofanywa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zake katika kipindi hiki cha mwaka mmoja cha Serikali ya Awamu ya Sita, pamoja na kuzingatia dhamira aliyoionyesha Mhe. Rais wakati akihutubia Bunge la 12 kwa mara ya kwanza zimedhihirisha kasi ya kiwango cha juu cha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025,

Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2021-2026) pamoja na maelekezo ambayo Mhe. Rais amekuwa akiyatoa katika Ofisi hii ambapo tumepata mafanikio makubwa katika maeneo yafuatayo:

i. Kusimamia mageuzi katika Utumishi wa Umma katika kutazama maslahi ya watumishi, ikiwemo suala la upandishaji vyeo na mishahara.
ii. Tumefanikiwa kuangalia upya Mfumo wa Wazi wa Upimaji wa Utendaji Kazi wa Watumishi (OPRAS) ili kupata mfumo sahihi wa usimamizi wa utendaji kazi wa Watumishi wa Umma nchini pamoja nakuimarisha mifumo ya uwajibikaji, ambayo itahakikisha Viongozi na Watumishi wa Umma katika ngazi zote wanawajibika kwa hiari katika kufikia malengo waliyojiwekea katika taasisi zao.
iii. Kuendelea kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Serikali Mtandao na kujenga mifumo ya TEHAMA inayohusu uendeshaji wa Serikali wa kila siku, kurahisisha utoaji wa huduma bora kwa umma na

kuimarisha maadili ya utendaji kazi katika utumishi wa umma kwa kutumia mifumo.

iv. Kuendelea kuhuisha sera na kanuni za Utumishi wa Umma ili ziendane na mazingira na mahitaji ya sasa ya ujenzi wa uchumi na maendeleo ya taifa.

v. Kujenga uwezo wa Viongozi na Watumishi wa Umma ili waweze kuwatumikia wananchi kikamilifu.

vi. Kubuni mbinu na mikakati ya kuhakikisha Watumishi wa Umma wanapata makazi bora kwa gharama nafuu.

vii. Kuendelea kusimamia upatikanaji wa rasilimaliwatu yenye sifa stahiki katika Utumishi wa Umma.

viii. Kuendelea kuhakikisha haki inatendeka kwa Watumishi wa Umma wenye malalamiko dhidi ya waajiri wao.

ix. Kuendelea kujenga mifumo imara ya utunzaji wa kumbukumbu, nyaraka na amali za taifa pamoja na kuimarisha mifumo ya utunzaji wa siri za Serikali kwa Viongozi na Watumishi wa Umma.

x. Kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa katika Utumishi wa Umma na taifa kwa ujumla.

xi. Kuendeleza juhudi za kupambana na umaskini na kuimarisha uchumi wa kaya maskini kupitia miradi mbalimbali.

***Ndugu Wanahabari;*** ninaomba sasa nianze kutoa ufafanuzi wa kina wa mafanikio yaliyopatikana ndani yam waka mmoja katika kila eneo kama nilivyoainisha hapo awali.

***Ndugu Wanahabari;*** katika eneo la Kusimamia mageuzi katika Utumishi wa Umma na kutazama maslahi ya watumishi, ikiwemo suala la upandishaji vyeo na mishahara, Mhe. Rais kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ametekeleza yafuatayo:

i. Mhe. Rais alituelekeza kuwapandisha vyeo/madaraja Watumishi 190,781 wenye sifa stahiki. Mhe. Rais aiamua tutumie jumla ya shilingi bilioni 39,649,988, 204 na kazi inaendelea.
ii. Kulipa madeni ya mishahara ya Watumishi wa Umma 65,394 yenye thamani ya shilingi bilioni 91,087,826,006.34

iii. Kuwabadilisha kada Watumishi wa Umma 19,386 na kuwalipa mishahara mipya yenye thamani ya shilingi bilioni 1,330,306,572.
iv. Kutoa vibali12,336 vya ajira mpya na mbadala ambapo jumla ya shilingi bilioni 7,761,869,809 zimelipwa.
v. Kuwapunguzia kodi watumishi wa umma kutoka asilimia 9 mpaka 8.

***Ndugu Wanahabari;*** katika kipindi hiki cha mwaka mmoja, Mhe. Rais kupitia Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma imefanikiwa kuanza kujenga Mfumo mpya wa Usimamizi wa Utendaji Kazi kwa Watumishi wa Umma (PEPMIS) ili kuondokana na changamoto za usimamizi wa utendaji kazi zilizojitokeza katika utekelezaji wa mfumo wa awali wa OPRAS, ambao haukuakisi hali halisi ya utendajikazi wa watumishi hali iliyoleta hisia za kupendeleana au kuoneana na kutokutumika kwa matokeo ya utendajikazi katika kufanya maamuzi ya kiutumishi. Mfumo mpya wa *Public Employees Management*

*Information System* (PEPMIS) utakuwa ni wa kielektroniki na utaondokana na matumizi ya makaratasi. Pia utaongeza uwazi katika usimamizi wa watumishi na kuondoa upendeleo na uonevu katika upimaji wa utendaji wa watumishi. Utaweka mifumo ya ufuatiliaji wa utendaji kazi wa watumishi kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa na yanayopimika. Mifumo huu pia utahamasisha uwajibikaji wa hiari na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za utendaji kazi wa watumishi.

Aidha, katika kipindi hiki Serikali imeanza ujenzi wa Mfumo mpya wa Usimamizi wa Utendaji kazi katika ngazi ya Taasisi *Public Institutions Performance Management Information System* (PIPMIS). Mfumo huu ni makubaliano ya kimaandishi kati ya Serikali na Taasisi ya Umma kuhusu malengo ambayo Taasisi husika itayatekeleza katika kipindi cha mwaka mmoja. Makubaliano hayo yatakuwa kati ya viongozi wakuu wa Taasisi na Viongozi wao wanaowasimamia katika masuala ya kisera na utendaji wa kila siku. Malengo yaliyomo ndani ya mikataba yatakuwa na vigezo,

shabaha na viashiria vitakavyotumika katika utendaji wa taasisi kila mwaka. Utekelezaji wa Mfumo wa Huu wa PIPMIS utaongeza uwajibikaji katika utekelezaji wa sera, mikakati na vipaumbele vya taasisi, sekta na taifa kwa ujumla; kuimarisha utamaduni unaojali matokeo; na kuleta matumizi bora ya rasilimali za umma. Manufaa haya yatatokana na kuwepo kwa vigezo na viashiria vya kupima utendaji wa taasisi katika maeneo hayo, kulinganisha na kushindanisha utendaji wa taasisi na kutoa Tuzo za utendaji mzuri kila mwaka.

***Ndugu Wanahabari;*** ili kupata mfumo sahihi wa kupima utendaji kazi wa Watumishi wa Umma na taasisi kama ilivyoelekezwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeunda timu ya Wataalam wabobezi ambao wameanza kutengeneza mifumo mipya ya kielektroniki ya usimamizi wa utendaji kazi wa Watumishi wa Umma na taasisi za umma.

***Ndugu Wanahabari;*** Ofisi ya Rais Menejementi ya Utumishi wa Umma imeendelea kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Serikali Mtandao na kujenga mifumo ya TEHAMA inayohusu uendeshaji wa Serikali wa kila siku na kurahisisha utoaji wa huduma bora kwa umma kama ifuatavyo:

i. Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imefanikiwa kujenga Mfumo wa Sema na Waziri wa UTUMISHI kwa lengo la kuwawezesha watumishi na wananchi kuwasiliana moja kwa moja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu masuala mbalimbali ya Utumishi na Utawala. Aidha mfumo huu unampa fursa Waziri wa Utumishi na Utawala Bora kufuatilia namna masuala ya utumishi na Utawala Bora yaliyowasilishwa na wananchi na watumishi wa Umma yalivyofanyiwa kazi na kumuwezesha Waziri kufuatilia hali ya uadilifu na uwajibikaji wa watumishi wa umma katika kushughulikia masuala mbalimbali ya utumishi na utawala bora. Mfumo huu pia unamuwezesha Waziri wa Utumishi na Utawala Bora

kuongea moja kwa moja na mlalamikaji ili kujua ni kwa namna gani tatizo lake limefanyiwa kazi na kuchukua hatua stahiki.

ii. Mfumo wa e-mrejesho ambao unapatikana kwa anuani ya e-mrejesho.gov.go.tz. Matumizi ya Mfumo huu yanawezesha wananchi kuwasilisha malalamiko, pongezi na maoni katika taasisi mbalimbali za Serikali na kupata nafasi ya kufuatilia malalamiko na maoni yaliyowasilishwa katika taasisi husika. Vilevile mfumo huu unawawezesha watumishi wa umma kuwasilisha maoni na malalamiko serikalini na kufuatilia mrejesho wa malalamiko yao.

iii. Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeanzisha Mfumo wa Dawati la Huduma kwa Mteja maarufu kama UTUMISHI Call Centre ambao unawawezesha wananchi na watumishi wa umma kupiga simu moja kwa moja kupitia namba 0262160240 kuelezea changamoto au lalamiko walilonalo. Mfumo huu hurekodi na kutunza kila suala lililowasilishwa. Huduma zinazotolewa na Call

Centre ni pamoja na ufafanuzi na ufuatiliaji masuala ya Upandishwaji Vyeo, Ubadilishwaji Vyeo, Uhamisho; Mishahara, Vibali vya Ajira, uidhinishaji wa makato na uhakiki wa Vyeti; Miundo ya Maendeleo ya Utumishi; Maadili; na Fursa za Mafunzo zinazotolewa na Wadau wa Maendeleo. Lengo la mfumo huu pia ni kupunguza gharama na kuokoa muda wa ufuatiliaji wa huduma hizo katika taasisi za umma na kuongeza uwajibikaji. Kwasasa kituo hiki kinapokea wastani wa simu 80 kwa siku.

iv. Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kipindi hiki imeamua kujenga Mfumo maalum wa Tathmini ya hali ya Rasilimaliwatu (Human Resource Management Assessment System) ambao unakusudia kukusanya, kutathmini na kuainisha mahitaji halisi ya watumishi kwenye Taasisi zote za Umma.

v. Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kipindi hiki pia imejenga Mfumo wa Huduma Mtandao kwa Watumishi (Watumishi Portal) ambao ni sehemu ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na

Mishahara (HCMIS). Mfumo huu ni mahsusi kwa Watumishi wa Umma kuweza kupata huduma mbalimbali za kiutumishi moja kwa moja bila kulazimika kwenda kwenye Ofisi za Waajiri wao. Mfumo huu pia unawawezesha watumishi wa Umma kuomba mkopo kutoka kwenye Taasisi za kifedha kwa njia ya Mtandao. Vilevile, watumishi wanaweza kutafuta watumishi wa kubadilishana vituo vya kazi kwenye mfumo, kuomba uhamisho kutoka kituo kimoja kwenda kingine au Taasisi moja kwenda nyingine.

vi. Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (WHMTH) imeanzisha mpango wa kuwa na vituo mahsusi vya kutolea huduma kwa wananchi vinavyojulikana kama **Vituo vya Huduma Pamoja**. Hadi mwezi Machi, 2022 vituo viwili (2) vya Huduma Pamoja vimeanzishwa katika majengo ya Posta Jijini - Dar es Salaam na Posta Jijini - Dodoma.

Huduma zilizoanza kutolewa katika Vituo hivyo ni pamoja na Huduma za RITA, Huduma za NIDA, Leseni za Biashara zinazotolewa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Huduma za Uhamiaji, Huduma za NSSF, Huduma za NHIF na Huduma za BRELA. Vituo hivi vya kutolea huduma sehemu moja vitaongeza ufanisi, ubora na urahisi wa kupata huduma zinazotolewa na Serikali.

vii. Sambamba na uanzishwaji wa Vituo vya Huduma Pamoja, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na WHMTH imeanza kuandaa mkakati kujumuisha makundi yenye mahitaji maalumu katika huduma za kidigitali zinakazotolewa na Serikali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022, kazi ya kukusanya mahitaji ya makundi hayo imeanza katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Taarifa zinazokusanya zinalenga kubainisha mahitaji ya makundi maalum ili kuyajumuisha katika mradi wa Tanzania ya Kidigitali.

***Ndugu Wanahabari;*** Katika eneo la uhuishaji wa Sera, Kanuni za Utumishi wa Umma na Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma katika kipindi hiki cha mwaka mmoja, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

i. Kuanza kufanya tathmini ya Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2008 kwa lengo la kuihuisha ili iweze kuendana na mahitaji na mazingira ya sasa katika usimamizi wa utawala na utumishi wa umma.
ii. Kuhuisha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 kwa lengo la kujumuisha marekebisho mbalimbali yaliyofanyika katika Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298.
iii. Kukamilisha kutafsiri Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 ili kurahisisha uelewa wa matumizi ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma.
iv. Kutokana na usimamizi mzuri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora na utekelezaji bora wa Mkataba wa Afrika wa Maadili na Misingi ya Utumishi

wa Umma na Utawala, Tanzania imeteuliwa kuwa moja kati ya nchi tano za Afrika ambazo zitashiriki katika tathmini ya utekelezaji wa mkataba huo.

***Ndugu Wanahabari,***

Katika kipindi cha mwaka mmoja, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia Taasisi ya Uongozi imetoa mafunzo ya uongozi kwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Viongozi wengine mbalimbali ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa ujumla mafunzo haya yamewaongezea viongozi hao uwezo wa kuchambua changamoto kwa kina, kuzitafutia ufumbuzi na kuboresha usimamizi wa rasilimali za Serikali ikiwa ni pamoja na rasilimaliwatu na rasilimali nyingine. Vilevile, katika kusogeza huduma za Chuo cha Utumishi wa Umma kwa wananchi wanaoishi mikoa ya Kanda ya Kati, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia Chuo cha Utumishi wa Umma imeanza ujenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Singida ambao ukikamilika watumishi wa umma na wananchi wa kanda hiyo watanufaika na uwepo wa huduma ya chuo hicho. Aidha,

ujenzi wa kampasi hiyo utaokoa kiasi cha shilingi milioni 87 zinazolipwa kwa ajili ya kupanga jengo la kuendesha shughuli za Chuo cha Utumishi wa Umma Kampasi ya Singida.

***Ndugu Wanahabari;*** katika kubuni mbinu na mikakati ya kuhakikisha Watumishi wa Umma wanapata makazi bora kwa gharama nafuu, katika kipindi hiki cha mwaka mmoja, Watumishi Housing imepata mafanikio yafuatayo;

i. Imeanza kutengeneza mfumo wa kuendesha mfuko wa revolving utakaosaidia ujenzi wa nyumba zenye gharama nafuu zitakazoweza kuwanufaisha wafanyakazi wa kada zote. Vilevile imetengeneza mpango kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutatua tatizo la makazi kwa watumishi kwa maeneo ya pembezoni.
ii. Katika kuwezesha watumishi wa umma na wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii kupata makazi bora na yenye gharama nafuu, Watumishi Housing inaendelea na ujenzi wa nyumba 80 katika eneo la Kisasa, Njedengwa jijini Dodoma.

***Ndugu Wanahabari;*** Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeendelea kuhakikisha inasimamia upatikanaji wa rasilimaliwatu yenye sifa stahiki katika ujenzi wa taifa. Katika kipindi hiki, Sekretarieti ya Ajira imefanikiwa kufanya yafuatayo:

i. Kujenga na kuzindua *"Ajira Portal Mobile App"* inayotumiwa kuendesha mchakato wa ajira Serikalini, ni *App* ambayo inaondoa vitendo vya rushwa na upendeleo kwa waombaji wa ajira, hivyo kuwezesha Serikali kupata watumishi wenye sifa stahiki.
ii. Kuanzisha Mfumo wa Kupima mienendo na tabia za wanaoomba nafasi za ajira Serikalini (Psychometric Test).

***Ndugu Wanahabari;*** Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia Tume ya Utumishi wa Umma imeendelea kuhakikisha haki inatendeka kwa Watumishi wa Umma wenye malalamiko dhidi ya waajiri wao.

Katika kipindi hiki imeshughulikia na kutolea uamuzi rufaa 313 na malalamiko 174 ya watumishi waliochukuliwa hatua na mamlaka zao za nidhamu.

***Ndugu Wanahabari;*** Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa imeendelea na jukumu la kujenga mifumo imara ya utunzaji wa kumbukumbu, nyaraka na amali za taifa pamoja na kuimarisha mifumo ya utunzaji wa siri za Serikali kwa Viongozi na Watumishi wa Umma. Katika kipindi hiki cha mwaka mmoja Idara hii imepata mafanikio yafuatayo:

i. Kuweka na kuhuisha Mfumo wa Utunzaji wa Kumbukumbu za Kiutendaji (Keyword Filing System) katika Taasisi za Umma hamsini na saba (57); na Mfumo wa Masijala Mtandao (e-File Management System) katika Taasisi za Umma ishirini (20).

ii. Katika kutekeleza maagizo ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu utunzaji wa siri za Serikali, Ofisi ya Rais, menejimenti ya Utumishi wa Umma imetoa Waraka wa

Utumishi wa Umma Na. 2 wa Mwaka 2021 kuhusu Mifumo Rasmi ya Mawasiliano Serikalini. Aidha, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa imefanya tathmini na ufuatiliaji wa mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma 152 kwa lengo la kujua hali halisi ya utunzaji kumbukumbu katika taasisi hizo. Vilevile, Idara imetoa elimu kwa taasisi za umma ili kuzikumbusha wajibu wao wa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utumiaji na utunzaji wa kumbukumbu.

iii. Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu cha Kanda ya Ziwa – Mwanza ambacho kina uwezo wa kuhifadhi jumla ya majalada 117,600 yaliyoko kwenye mfumo wa karatasi. Aidha, Kituo hicho kimewekewa miundombinu wezeshi ya kuhifadhi nyaraka kidigitali na ununuzi wa vifaa vya kuhifadhi nyaraka katika mifumo hiyo ya kidigitali unaendelea.

iv. Kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbuku na vitu vya Waasisi wa Taifa kutoka katika Taasisi za Umma na watu binafsi ili kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu. Vilevile Idara imekusanya jumla

ya kumbukumbu 821 za Waasisi wa Taifa (Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume) kwa ajili ya matumizi ya vizazi vya sasa na vijavyo kwa maendeleo ya taifa.

***Ndugu Wanahabari;*** Ofisi ya Rais Utawala Bora kupitia TAKUKURU na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, imefanikiwa kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa katika Utumishi wa Umma na taifa kwa ujumla pamoja na kuimarisha maadili ya viongozi na kupata mafanikio yafuatayo:

i. Taarifa ya utafiti iliyofanywa na Transparency International ya mwaka 2021 katika kiashiria cha *Corruption Perception Index* (CPI) kinaonesha kuwa Tanzania imeendelea kufanya vizuri kwa kupata alama 39 na kushika nafasi ya 87 kati ya nchi 180, ikiwa imepanda kwa nafasi 7 ikilinganishwa na nafasi ya 94 ya mwaka 2020. Nchi yetu imeshika nafasi ya pili kwa Ukanda wa Afrika Mashariki katika kiashiria hicho cha CPI.

**ii.** Ofisi ya Rais Utawala Bora kupitia TAKUKURU imefanikiwa kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika miradi ya maendeleo 1297 yenye thamani ya shilingi trilioni 5.094 katika sekta za Afya, Elimu, Fedha, Nishati, Ujenzi, Maji, Uvuvi, Maliasili na sekta ya Kilimo. Matokeo ya ufuatiliaji huo yalibainisha miradi 133 yenye thamani ya shilingi bilioni 55.6 kuwa na kasoro mbalimbali na kuanzishiwa uchunguzi.

iii. Vilevile, TAKUKURU kupitia operesheni zake mbalimbali imefanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi 3,017,926,501.6.

iv. Imefanikiwa kukamilisha uchunguzi wa majalada 592 na kufungua kesi mpya 296 mahakamani. Aidha, kesi 401 ziliamuliwa mahakamani.

v. Katika kutekeleza agizo la Mhe. Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha Mifumo ya TEHAMA ndani ya Serikali inawasiliana na kubadilishana taarifa ili kupunguza mianya ya rushwa na gharama za utoaji huduma, Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) imekamilisha kutengeneza Mfumo unaojulikana kama ***Government Enterprise Service Bus (GovESB)***

mfumo ambao unaiwezesha Mifumo mbalimbali ya Serikali kubadilishana taarifa.

vi. Kuanza ujenzi wa jengo la ghorofa sita la Ofisi ya TAKUKURU makao makuu Dodoma ambapo ujenzi umefikia hatua ya ghorofa ya kwanza.

vii. Ofisi ya Rais Utawala Bora kupitia Sekretarieti ya Maadili imeanzisha klabu mpya za maadili 44. Kati ya klabu hizo**,** 19 ni za shule za msingi, 19 shule za sekondari na klabu sita ni za vyuo. Klabu zote kwa pamoja zina jumla ya wanachama 1,850. Uanzishaji wa klabu hizi katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya elimu ya juu unalenga kuandaa viongozi waadilifu katika vizazi vijavyo.

viii. Kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tano la Makao Makuu ya Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili Dodoma ambapo ujenzi umefikia kiwango cha asilimia 50.

ix. Katika kuimarisha utendaji kazi wa TAKUKURU na kuwa na rasilimaliwatu inayokidhi mahitaji, Serikali ya Awamu ya Sita imetoa kibali cha ajira za watumishi 350.

***Ndugu Wanahabari;*** Ofisi ya Rais Utawala Bora kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge (MKURABITA) imeendeleza juhudi za kupambana na umaskini na kuimarisha uchumi wa kaya maskini kupitia miradi mbalimbali. Katika kipindi cha mwaka mmoja, taasisi hizo zimepata mafanikio yafuatayo:

**i.** Kukamilisha utambuzi na uandikishaji wa kaya ambazo hazikufikiwa wakati wa utekelezaji wa Kipindi cha Kwanza cha Mpango.

   Jumla ya Kaya 602,672 zimetambuliwa kutoka katika vijiji 7,217 ambapo kati ya hizo, kaya 494,348 (82.0%) zimekidhi vigezo vya umaskini na kuingizwa kwenye Mpango. Kaya hizi pia zimepokea ruzuku kwa mara ya kwanza mwezi Januari 2022.

**ii.** Kuibua miradi 724 ya sekta za elimu, afya, maji, kilimo, barabara za vijijini, hifadhi ya mazingira, masoko na miradi ya kuongeza kipato. Miradi hii ya kuongeza kipato iliyoibuliwa ina thamani ya shilingi

bilioni 33.3 na imetekelezwa na jamii katika halmashauri 33 nchini.

**iii.** Kuundwa kwa vikundi 30,648 vya Kuweka Akiba vyenye Wanachama 421,353 ambapo vikundi hivyo vimeweka akiba ya shilingi bilioni 6.2. Vikundi hivyo vimewezesha wanachama kukopeshana shilingi bilioni 2.9 ili kuanzisha au kuendeleza miradi ya kuongeza kipato.

**iv.** Kutambua na kuandikisha watu wenye ulemavu ndani ya kaya za walengwa. Jumla ya watu wenye ulemavu 34,001 (wanaume 95,442 na wanawake 38,559) wametambuliwa ili kuingizwa kwenye Mpango.

**v.** Kuimarisha shughuli za kiuchumi zilizoathirika zaidi kutokana na UVIKO-19 kupitia shilingi bilioni 5.5 za Kampeni ya Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Fedha hizi zilitumika kulipa ujira kwa kaya za walengwa 40,740 ambao walitekeleza miradi ya jamii kupitia programu ya Ajira za Muda kwa Walengwa.

**vi.** Kuwezesha wanafunzi zaidi ya 1200 wanaotoka kaya za walengwa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wenye sifa za kuingia katika vyuo vinavyotoa elimu ya juu kunufaika na mkopo wa elimu ya juu kwa asilimia 100. Mikopo hiyo inatokana na TASAF kuingia makubaliano (MoU) na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

**vii.** Ndugu Wananchi katika kipindi cha Mwaka mmoja Mheshimiwa Rais amewezesha Taasisi ya MKURABITA kupatiwa Shilingi Bilioni 3.2 ili kuendeleza miradi ya urasimishaji mali za Wanyonge katika ardhi na biashara na hivyo kukamilisha miradi ambayo imewezesha yafuatayo:-

- Mheshimiwa Rais amewezesha wakulima 2,409 wa vyama vya ushirika 5 kutumia hatimiliki za ardhi kama dhamana na kupata mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 28.2 kupitia Mpango wa MKURABITA.

- Mheshimiwa Rais amewezesha wafanyabiashara waliopatiwa mafunzo na MKURABITA kukopa zaidi ya Shilingi Bilioni 9.38 katika kuongeza mitaji yao.

- Mheshimiwa Rais kupitia MKURABITA amewezesha asilimia 2 ya wamiliki wa majengo, asilimia 1 ya wamiliki wa mashamba na asilimia 1 ya wamiliki wa viwanja wa Tanzania wametumia rasilimali zao kukopa kiasi cha Shilingi trilioni 1.06 kutoka Taasisi za fedha.
- Mheshimiwa Rais kupitia fedha alizozitoa MKURABITA amesaidia kupunguza migogoro ya ardhi kwa asilimia 64 ya migogoro 25,409 iliyobainiwa na MKURABITA iliyoibuliwa na MKURABITA.
- Mheshimiwa Rais kwa kuiwezesha MKURABITA amesaidia upatikanaji wa ajira 44,387 zilizotokana na miradi ya urasimishaji wa ardhi na biashara.

***Ndugu Waandishi wa Habari;*** Mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, nichukue fursa hii kuwashukuru tena kwa kazi nzuri mnayoifanya kwa kushirikiana na ofisi yangu katika kuuhabarisha umma juu ya masuala ya utumishi wa umma na utawala bora yanayotekelezwa na ofisi yangu.

***Ndugu Waandishi wa Habari;*** Binafsi niwahakikishie kuwa, ofisi yangu itaendelea kushirikiana nanyi ili umma wa watanzania upate habari sahihi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi yangu ili wananchi wanufaike na huduma zinazotolewa katika taasisi zote za umma nchini.

Niwasihi kwa pamoja tuunge mkono kwa vitendo kaulimbiu ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ya KAZI IENDELEE ili taifa lipige hatua kimaendeleo.

***"ASANTENI KWA KUNISIKILIZA"***